

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

621

MBINU ZA KUFUNDISHIA KISWAHILI

MUDA: Saa 3

Alhamisi Novemba 06, 2003 Mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **YOTE** katika sehemu A na B, na maswali **MAWILI (2)** kutoka sehemu C.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

SEHEMU A (Alama 36)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Eleza kwa ufupi shughuli tatu zilizosaidia kukuza lugha ya Kiswahili kabla ya uhuru wa Tanganyika.
2. Taja mashina manne ya vitenzi na andika mzizi na kiambishi tamati kinachohusika kwa kila shina la kitenzi ulichotaja.
3. Bainisha makosa yaliyomo kwenye sentensi zifuatazo kwa kuziandika kwa usahihi.
 - (a) Ana aliwakilisha ripoti kwa mkuu wake wa kazi.
 - (b) Ili niweze kufaulu vizuri mtihani huu, ni budi kujibu maswali kwa makini.
 - (c) Juma alituma Zena dukani.
 - (d) Mgagagigikoko ameambukizwa UKIMWI.
4. Taja vifaa vikuu vitatu vya mtaala vitumikavyo kufundishia somo la Kiswahili.
5. Fafanua maana ya Kiima (K) na Kiarifu (A). Toa mfano mmoja wa Kiima na mmoja wa Kiarifa kwa kutumia sentensi sahili.
6. Wasaidie wanafunzi wa darasa la saba kubainisha aina za kauli zinazojitokeza katika tungo zifuatazo:
 - (a) Amemsaidia kalamu
 - (b) Amepigwa sana
 - (c) Mto haupitiki
 - (d) Ameshutumiwa vikali.
7. Eleza njia tatu unazoweza kutumia kuwafundishia watoto wa Darasa la Kwanza kusoma.
8. Yapo maneno ya lugha nyingine yaliyoingizwa na kutumika katika lugha ya Kiswahili. Oanisha maneno ya Kiswahili yaliyopo kwenye Fungu B na lugha inayohusika katika Fungu A.

Fungu A	Fungu B
(a) Kiingereza	(i) ghali, shujaa
(b) Kireno	(ii) embe, jangili
(c) Kiarabu	(iii) nanasi, meza
(d) Kichina	(iv) dereva, shati
(e) Kihindi	(v) chai, chungwa

9. Taja mbini shirikishi kumi uzijuazo za kufundishia somo la Kiswahili.

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **YOTE** katika sehemu hii.

10. Eleza mambo manne muhimu yaliyofanyika na ambayo yalisaidia kuendeleza lugha ya Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza.
11. Eleza mambo muhimu ya kuzingatia katika kuwasundisha wanafunzi wa Darasa la Saba utungaji wa Insha.

SEHEMU C (Alama 24)

Jibu swali **MOJA (1)** kutoka sehemu hii.

12. Umealikwa kwenye semina ya Wasifu wa Lugha ya Kiswahili ili ukatoe mada kuhusu ithibati ya kwamba lugha hiyo ni ya Kibantu na si Kiarabu. Bainisha vipengele vitakavyohusika katika mada yako.
13. Andika barua ya kikazi ya kuomba kujiunga na masomo ya Sekondari Kidato cha Kwanza ili iwe kama zana ya kufundishia wanafunzi wa Darasa la Saba uandishi wa barua ya aina hiyo.
14. "Nahau, methali na vitendawili ni tanzu za fasihi simulizi zilizo na maana inayofanana". Jadili kauli hiyo kwa kutoa mifano kwa wanafunzi wako wa Darasa la Sita.
15. Mjadala ni moja ya mbinu za kufundishia Kiswahili. Eleza:
 - (a) Maana yake
 - (b) Jinsi inavyotumika
 - (c) Faida tatu (3) za mbinu hiyo
 - (d) Dosari tatu (3) za mbinu hiyo.

5/11/2023
Majlis Ushirikiano
Sauti ya Taifa
St. 2, 5722
Dar es Salaam
Tanzania
Tel: +255 22 222 1234
Email: info@ust.tz